

MASHARTI YA KUJIUNGA NA UTUMISHI WA UMMA.

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma.

1.0 *Utangulizi.*

Ndugu Msomaji, katika Ijumaa ya wiki iliyopita tuliangalia makala iliyohusu Ajira katika Utumishi wa Umma itazingatia sifa. Katika makala hiyo tulieleza kuwa watu wanaotakiwa kufanya kazi katika utumishi wa umma ni wale tu wenye taaluma, uwezo, ubunifu na uhodari, sifa ambazo zinapaswa kuambatana na uaminifu, uadilifu na uwajibikaji. Aidha, tulieleza kuwa watumishi wenye sifa kama hizo ndiyo msingi au nyenzo kuu katika ujenzi wa uchumi wa kisasa. Uchumi wa kisasa hauwezi kujengwa na rasilimali watu isiyo na sifa zinazoendana na mabadiliko mbali mbali ya kiuchumi, kisiasa kiteknolojia n.k.; hivyo mamlaka zinazohusika na masuala ya ajira zinapaswa kuzingtia kikamilifu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazoendesha masuala ya ajira. Katika makala ya leo, tutaangalia masharti yanayopaswa kuzingtiwa na mamlaka zinazohusika na ajira wakati wa kutekeleza jukumu la ajira katika utumishi wa umma ili kujenga mazingira mazuri ya utoaji wa huduma kwa wananchi. Mamlaka zinazoshughulikia masuala ya ajira zina changamoto ya kuhakikisha masharti ya kujiunga na utumishi wa umma yanazingatiwa ipasavyo. Masharti hayo ni pamoja na Elimu,

tabia njema, ajira ya raia wa kigeni iwapo raia wenye sifa zinazotakiwa hawapo, umri wa kuingia na kuacha kazi katika Utumishi wa Umma na Afya ya mtu au ulemavu wa viungo.

2.0 *Masharti.*

Katika lugha ya kawaida neno 'masharti' ni wingi wa neno sharti. Neno hili linaweza kutafsiriwa kama kanuni [rule] ambayo inamwezesha mtu kuamua/kufanya au kufuata jambo fulani katika utekelezaji wa majukumu au kazi fulani. Katika utumishi wa umma neno masharti linaweza kutafsiriwa kama utaratibu unaomwezesha mwenye mamlaka katika utumishi wa umma kuamua utekelezaji wa kazi fulani. Hivyo tunapoangalia masharti ya kujiunga na utumishi wa umma katika mtazamo huo, tunaweza kutafsiri neno masharti kuwa ni taratibu ambazo, wenye mamlaka ya ajira zinawawezesha kuchagua au kuteua watu wanaotakiwa kujiunga na utumishi wa umma. Masharti hayo ni kama yafuatayo:

2.1 *Elimu.*

Kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999, kiwango cha chini cha kumwezesha mtumishi kuajiriwa kwa masharti ya kudumu katika utumishi wa umma kitakuwa elimu ya Kidato cha IV.

2.2 *Tabia njema.*

Ili kuajiriwa katika utumishi wa umma itahitajika mtumishi awe mwenye tabia njema.

2.3 *Umri.*

Umri wa chini wa kuingia katika utumishi wa umma utakuwa miaka 18 na umri wa juu wa kuacha utumishi wa umma ni miaka 60.

2.4 *Afya.*

Afya ya mtu au ulemavu wa viungo hautamzuia mtu kuajiriwa katika utumishi wa umma isipokuwa tu kama hali hii itaathiri moja kwa moja utendaji wa kazi inayohusika.

2.5 *Rais wa kigeni.*

Raia wa kigeni watafikiriwa kuajiriwa katika utumishi wa umma iwapo raia wenye sifa zinazotakiwa hawatapatikana. Watu hao wataajiriwa kwa masharti ya mkataba wa muda maalum usiozidi miaka 3 na kwa kibali cha Mkuu wa Utumishi wa Umma.

3.0 *Hitimisho.*

Uzingatia wa taratibu katika uendeshaji wa ajira katika utumishi wa umma ni jambo la msingi sana. Waliopewa mamlaka ya kushughulikia ajira wana changamoto ya kuhakikisha kuwa taratibu zinazingatiwa ili utumishi wa umma uwe na rasilimali watu yenye sifa zinazotakiwa na ambayo inaweza kuachangia kwa kiasi kikubwa katika harakati za kupambana na umaskini na kukuza uchumi wa nchi.

Ikiwa una maoni/ushauri au maswali tafadhali tuandikie.

Katibu,
Ofisi ya Rais,
Tume ya Utumishi wa Umma,
S.L.P. 9143,
DAR ES SALAAM.

Au Piga simu: 022-2126811/4